

Chanjo za Ziada za COVID-19 Sasa Inapatikana

Dozi za chanjo ya ziada kwa aina zote tatu za chanjo za COVID-19 sasa zinapatikana. Ikiwa unastahiki, unaweza kuchagua ni aina gani ya chanjo utapata kama dozi ya ziada. Kupata dozi ya ziada ya chanjo zozote za COVID-19 ambazo kwa sasa zimeidhinishwa Marekani kutaongeza kinga yako dhidi ya COVID-19 na aina zake, kama Delta. Watu watachagua kwa jumla kupata aina sawa ya chanjo waliyopata hapo awali, lakini wanaweza kuchagua kupata aina tofauti ya chanjo ya ziada. CDC inaruhusu aina hii ya “kucganganya na kulinganisha” kwa dozi za ziada.

Moderna na Pfizer

Unastahiki kupata chanjo ya ziada ikiwa tayari umepokea dozi zote mbili za Moderna au Pfizer **angalau miezi sita iliyopita na:**

- Una umri wa miaka 65 au zaid.
- Una umri wa miaka 18 au zaidi na upo katika hatari ya juu ya kupata COVID-19 kali; au
- Una umri wa miaka 18 na zaidi na unaishi au kufanya kazi katika mazingira yenye hatari ya juu.



J&J

Unastahiki kupata chanjo ya ziada ikiwa tayari umepokea dozi moja ya Johnson & Johnson (Janssen) **angalau miezi miwili iliyopita na una:**

- Umri wa miaka 18 au zaidi.

Wakazi wa Rhode Island wanaostahiki sasa wanaweza kupata miadi ya aina zote tatu za dozi za ziada kwa kutembelea [VaccinateRI.org](https://www.vaccinateRI.org) au kupiga **844-930-1779**. Pia unaweza kujifunza zaidi kuhusu chanjo za COVID-19 na mahali pa kupata miadi katika [C19VaccineRI.org](https://www.c19vaccineRI.org).

Ukiwa na maswali kuhusu ni chanjo gani ya ziada ni bora kwako, tafadhali onga na mhudumu wako wa afya.



11/4/2021